

NOTISI KWA UMMA

SHERIA YA MIPANGILIO YA MIJI NA MATUMIZI YA ARDHI

NAMBARI 13 YA 2019 - FOMU PLUPA L-2 (r.10)

NOTISI KUHUSU KUKAMILIKA KWA UTAYARISHAJI WA RAMANI YA MPANGILIO WA MAENDELEO

**Aina ya Ramani ya Mpangilio
wa Maendelo/Ukuzaji:**

**RAMANI YA USTAWI WA SEHEMU-NAMBARI:
LMU.231.IV.1.04-SEHEMU ILIYOJENGWA KITUO
KIDOGO CHA KAMPUNI YA KENYA POWER
CHA KUSAMBAZA UMEME - MOKOWE.**

NOTISI inatolewa hapa kwamba utayarishaji wa Ramani ya Sehemu ya Ustawi iliyotajwa hapo juu ulikamilishwa mnamo **Machi 1, 2022**.

Nakala ya ramani iliyotayarishwa imewekwa kwa ukaguzi wa umma bila malipo katika Afisi ya Waziri wa Ardhi, Mipangilio ya Miji, Maendeleo ya Miji, Miundo Misingi na Kawi - Mokowe, Kaunti ya Lamu kati ya saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni (**8.00 am-5.00 pm**) kutoka siku ya Jumatatu hadi Ijumaa.

Mtu yeyote aliye na haja ya kuwasilisha maoni yake au pingamizi kuhusiana na Ramani hii anaweza kufanya hivo kwa kumwandikia Waziri husika wa Ardhi na Mipangilio ya Miji, **S.L.P. 74-80500 Lamu**. Maoni au pingamizi ziweze kuwasilishwa ndani ya siku sitini (60) kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa notisi hii. Maoni au pingamizi ziandamanishwe na sababu zake.

AHMED M. HEMED

WAZIRI WA KAUNTI

**IDARA YA ARDHI, MIPANGILIO YA MIJI, MAENDELEO YA MIJI
MIUNDO MISINGI NA KAWI**

Tarehe: Agosti 9, 2022